1. **Swali:** ***Umuhimu wa takwimu kwa jamii na Taifa unajulikana, NBS wamesema kwamba mojawapo ya changamoto zao ni uhaba wa rasilimali. Je, wanathibitisha vipi kwamba katika hali hii wanatupatia takwimu sahihi? Wanafanya juhudi gani kukabiliana na changamoto hii? (Emmanuel Magoa – ILO).***

**Jibu:** Uhaba wa rasilimali ni mojawapo ya changamoto zinazoikabili Ofisi ya Taifa ya Takwimu lakini changamoto hii haiwezi kuharibu au kuingilia mfumo imara uliopo wa ukusanyaji wa takwimu bora nchini. Watumishi wachache waliopo wanasaidiana na wadadisi ambao hupewa mafunzo ya jinsi ya kukusanya takwimu chini ya wasimamizi wenye sifa stahiki ili kuhakikisha takwimu bora zinapatikana. Aidha, serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo wanasaidia katika kukabiliana na ukosefu wa rasilimali fedha, hivyo kiasi kinachopatikana kinapangiliwa ipasavyo ili kukidhi mahitaji ya wadau wa takwimu nchini.

2. **Swali:** ***Kuna mikakati gani juu ya usambazaji wa Watakwimu katika kila ngazi yaani kijiji, kata, wilaya hadi mkoa ikiwa wanaosomea takwimu ni wachache na hawana***

**Jibu:** Kwa sasa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina ofisi katika kila mkoa. Ofisi hizo zinaongozwa na Mameneja wa Takwimu. Mameneja hawa wana vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na magari ambayo huwasaidia kufika hata maeneo ya vijijini kusimamia shughuli za kitakwimu. Takwimu zilizokamilika husambazwa kwa wadau mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya hadi Vijijini kupitia machapisho mbalimbali, mikutano ya watoa takwimu, watumiaji wa takwimu, n.k.

3. **Swal**i: ***Kwa nini kazi za kitakwimu zinafanywa na mtu yeyote tofauti na taaluma zingine? NBS imejipanga vipi kwa hilo? – EASTC***

**jibu:** Kwa sasa, kazi za ukusanyaji takwimu zinafanywa na mchanganyiko wa watakwimu na wasio watakwimu wa kusomea lakini kabla ya kuanza zoezi lolote la ukusanyaji takwimu, wadadisi huwa wanapewa mafunzo kuhusiana na aina ya utafiti/kazi husika na maada ya mafunzo hupelekwa kwenye mazoezi kwa vitendo ili kuhakikisha wanaelewa vyema misingi ya ukusanyaji wa takwimu bora. Aidha, kazi ya uchambuzi wa takwimu hufanywa na wataalamu wa takwimu waliosomea. Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina mpango wa kuwatumia wahitimu wa cheti na diploma toka chuo cha takwimu changanyikeni kama wadadisi kwani wanakuwa na ujuzi na mbinu za jinsi ya kukusanya takwimu, na hii itapunguza gharama kwani kutoa mafunzo kwa wadadisi wasio na taaluma ya takwimu ni ghali.

**4. Swali:** ***Kama takwimu bora zinatokana na kukusanywa na wataalam. Je, ukusanyaji wa takwimu na watu wasio wataalam unachangiaje kushusha ubora wa takwimu? Je NBS wamejipangaje kuongeza wataalamu? – Victoria Maro – EASTC, Ndunguru Alfred – Kibaha (5,7)***

**Jibu:** Ni kweli kwamba ukusanyaji wa takwimu kwa kutumia wadadisi ambao sio wataalamu unaweza kushusha ubora wa takwimu zitakazokusanywa. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kuhakikisha takwimu zinazokusanywa ni sahihi na zina ubora kwa kuwapatia mafunzo wadadisi ambao sio wataalamu kabla ya kuwaajiri kweye kazi ya kukusanya takwimu. Kwa kawaida mafunzo wanayopata wadadisi ni ya nadharia na vitendo, na wakati wa kukusanya takwimu huwa kuna msimamizi ambaye huzungukia kila mdadisi na kusikiliza jinsi anavyohoji, kisha hupitia madodoso yote ili kuyahakiki kabla ya kuyapeleka sehemu husika kwa ajili ya kuingiza taarifa kwenye kompyuta na kuzichambua. Wakati wa kutayarisha dodoso huwa kuna maswali maalumu (control questions) ambayo humwongoza msimamizi kuangalia mtiririko wa maswali na majibu, hivyo vigezo vya kudhibiti ubora huzingatiwa katika hatua zote kuanzia hatua ya uandaaji wa dodoso, ukusanyaji wa takwimu, uingizaji kwenye kompyuta, n.k.

**5. Swali;** Idara nyingi na baadhi ya Taasisi za Serikali zimekuwa zikikusanya takwimu kupitia watu ambao sio watakwimu na hao huchangia takwimu kuwa mbovu. Je, NBS tumejipanga vipi kukabiliana na shida hii ili kuboresha takwimu? **Ndunguru Alfred – Kibaha**

**Jibu**; Rejea jibu la swali la 5 juu

6. **Swali**; Serikali imekuwa nzito kidogo katika kutumia tafiti zinazofanywa na taasisi nyingine kama taarifa na tafiti kutoka BEST na tume mbalimbali." sasa kama watakwimu tufanyaje ili kuondokana na hili tatizo kwa maendeleo ya nchi? – **Kalinga**

**Jibu:** Uamuzi wa kutumia au kutotumia takwimu ya aina fulani ni wa mtumiaji mwenyewe. Ili mdau/mtumiaji wa takwimu aweze kuamua atumie takwimu ipi ni muhimu aichunguze kwanza takwimu anayotaka kutumia, imetayarishwaje, kama inakidhi viwango vya kimataifa, ni sahihi, inaweza kulinganishwa na takwimu nyingine kama hizo toka vyanzo tofauti, n.k. Mtakwimu anapopewa takwimu toka kwenye kumbukumbu za kiutawala, anashauriwa atafute takwimu hiyo toka chanzo zaidi ya kimoja ili aweze kulinganisha na kama haridhiki basi awaone wale waliotayarisha takwimu hizo kwa ufafanuzi zaidi, kwani wakati mwingine makosa ya kibinadamu hutokea wakati wa kutayarisha takwimu.

Serikali imekuwa nzito kutumia takwimu zilizotayarishwa na taasisi nyingine nje ya NBS sababu mara nyingi takwimu hizo hazitayarishwi kwa kutumia mifumo iliyokubalika kimataifa na hivyo hazina viwango. Serikali inaziamini zaidi Takwimu zilizotayarishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu sababu ndio taasisi pekee Tanzania inayotoa takwimu rasmi na ambazo zina viwango na ubora unaokubalika kimataifa. Ili kuondokana na changamoto ya kutumia takwimu zinazokinzana, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inawashauri watafiti kufanya tafiti shirikishi ili kuipa nafasi NBS kuwaongoza kitaalamu katika kila hatua ya utafiti kwa matokeo mazuri ya utafiti husika.

**7. Swali;** ***Upatikanaji wa takwimu sahihi ni pamoja na kupata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa mtoa taarifa, watu wengi hawapendi kutoa taarifa za ukweli kwa sababu hawajui umuhimu wa takwimu, Je serikali ina mkakati gani?***

**Jibu:** Kwa kiasi kikubwa, ubora wa takwimu unategemea mambo mengi, ikiwemo usahihi wa taarifa zinazotolewa na wahojiwa. Ushirikiano wa mtoa taarifa nao unategemea jinsi ambavyo amehamasishwa au uelewa wake kuhusu taarifa anayotakiwa kuitoa. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inajitahidi kuwaelimisha wadau wake kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikutano (user-producer workshops), vipindi vya Redio na Luninga, na mikusanyiko mingine kama huu wa leo ambapo maana na umuhimu wa kutoa takwimu bora huelezwa. Hata hivyo uhamasihaji na uelimishaji jamii kuhusu umuhimu wa takwimu ni zoezi endelevu kwani tasnia ya takwimu inakua na mbinu za kitakwimu nazo zinatakiwa ziendane na wakati. Pia kutokana na sheria ya takwimu, NBS huwa inaiwahakikishia jamii usiri wa taarifa wanazotoa. Hizi zote ni jitihada za kuwafanya wadau watoe taarifa sahihi na zenye ubora.

**8. Swali:** ***Kuna asasi za kiraia zinazotoa takwimu, na wakati mwingine zinaleta mtafaruku katika jamii. Je, NBS ikiwa ni mamlaka husika in mkakati gani / sheria kuzuia takwimu zisizo sahihi.*** **– Ummi – Ihi**

**Jibu:** Ni kweli kumekuwa na tatizo hili, kimsingi matatizo haya yanatokana na taasisi kutofuata sheria inayotaka taasisi zote zinazofanya tafiti kuihusisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kuhakiki mbinu na viwango vilivyotumika katika kutayarisha takwimu husika. Kwa sasa NBS haina meno kisheria kuwabana watoa taarifa kama hizo ila serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu iko kwenye mchakato wa kuandaa muswada mpya wa sheria ya takwimu ambayo pamoja na mambo mengine itasaidia kutatua tatizo hili na hivyo kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi.

9. **Swali: Je, Takwimu zinazotolewa na television au asasi nyingine katika kupima utendaji wa viongozi zinafuata vigezo vya kitakwimu? Kama sio, nini kifanyike?**

**Jibu:** Kimsingi Takwimu zinazotolewa kwenye Luninga mfano zile za 'KIPIMA JOTO; sidhani kama zinafuata vigezo vya kitakwimu sababu sampuli inayotumika kutoa hayo matokeo haijaandaliwa kitaalamu na mbinu zinazotumika kuchanganua na kutoa matokeo hayo hazijulikani. Kimsingi maoni ya watu 10 hayawezi kuwasilisha maoni ya watu milioni 44. Aidha Takwimu zinazotolewa na asasi nyingine kwa matumizi yao inawezekana zinafuata vigezo vilivyowekwa na asasi husika lakini mara nyingi sio vigezo vya kitakwimu vilivyokubalika kimataifa. Tunasisitiza tena kwamba Takwimu zipo nyingi na za kila aina lakini takwimu RASMI inapatikana Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Hata hivyo, Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP) umeandaliwa ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za ukusanyaji na uchambuzi wa Takwimu nchini. Mpango huu una miaka mitatu sasa na utaendelea mpaka mwaka 2016. Mafanikio yake ni pamoja na kuwaleta karibu watumiaji na wazalishaji wa Takwimu nchini. Kuboresha miundombinu, kutoa machapisho, kuelimisha wizara, idara taasisi mbalimbali za serikali jinsi ya kutumia mbinu na kukokotoa takwimu rasmi nchini (standards and methods), vitendea kazi mfano magari na kompyuta.

Mpango wa TSMP umelenga katika maeneo muhimu matano ambayo ni;

- Uboreshaji wa miundo ya taasisi na sheria ya takwimu,
- Uendelezaji na uboreshaji raslimali watu, Uimarishaji wa miongozo ya ukusanyaji takwimu,
- Kuimarisha upatikanaji na usambaji wa takwimu na
- Upatikanaji wa majengo ya ofisi na vitendea kazi.

Hivyo wadau wa takwimu tushirikiane ili kupata takwimu bora

**10. Swali:** Hongera sana NBS, walipa kodi watabanwaje kulipa kodi TRA kama ilivyokusudiwa? (Mkurugenzi wa East African Nguvukazi and Juakali Partners).

**Jibu:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina mfumo wa Geographical Information System (GIS) ambao ukitumiwa unaweza kuonesha sura ya nchi katika ramani na maeneo ya watu na biashara. Mfumo huu ukiunganishwa na mifumo ya Brella na TRA basi itakuwa rahisi kwa TRA kuwajua na kuwafuatilia walipa kodi wake. Hata hivyo ieleweke kuwa swala la kuwabana walipa kodi ni la TRA na sio NBS.

**11. Swali**; ***Tulisikia kwamba kuna Sheria ya Takwimu itakayopitishwa na Bunge lililopita. Je, Sheria hiyo imepitishwa?***

**Jibu**: Sheria mpya ya takwimu bado ipo kwenye mchakato na kimsingi inazungumzia mambo mazuri kwa ajili ya kuboresha Tasnia ya Takwimu. Kwa upande wa Serikali mchakato umeshakamilika na tunategemea muswada wa Sheria hiyo utasomwa kwenye Bunge lijalo la mwezi wa kumi na mbili kama kusipokuwa na mabadiliko.

***12. Swali (a): Mheshimiwa Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi na Mipango, Je, hauoni umuhimu wa kusaidia uundwaji wa Bodi ya Watakwimu ili iweze kuratibu ubora na usajili wa wataalamu? (Marcel – TCRA)***

**Jibu (a):** Uuundwaji wa Bodi ni jambo la muhimu sana na tumechelewa kwa kuwa hii ni mingoni mwa taaluma adimu (rare profeesional)  na kwa kuwa kuna watakwimu wachache yawezekana ndio maana chombo hiki kimechelewa. Wito wangu kwa watakwimu ni kwamba wao wenyewe waone umuhimu wa kuanzisha mchakato huu badala ya kusubiri kuanzishiwa. Wataalam waanzishe mchakato na kushirikisha wadau wote kuona jinsi ya kuunda chombo hiki muhimu.

**Swali (b**): ***Je, unawezaje kusaidia kuishauri Serikali katika kutumia wataalam wa takwimu katika ngazi mbalimbali za uongozi hapa Tanzania? Kwa sasa mtu yeyote anaweza kutumiwa kama mtakwimu bila kujali elimu yake.***

**Jibu (b):** Hili ni jambo zuri ila changamoto ni kuwa bado kuna watakwimu wachache nchini, na ndio maana serikali imeongeza nguvu ya kuwaelimisha watu zaidi kupitia Chuo cha Takwimu mashariki mwa Afrika ili kupata wataalam wa takwimu katika kila ngazi mbalimbali za utawala na kuwatumia ipasavyo katika sehemu mbalimbali nchini.

***13. Swali: NBS wanawatumiaje watakwimu waliopo kwenye Halmashauri katika kukusanya na kusambaza takwimu? ( Daudi Chambo – Kinondoni Municipal).***

**Jibu:** Watakwimu wa Halmashauri wanatumika kwenye ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu. Mfano, Katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Mpango wa baadaye wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni kufungua Ofisi za Takwimu katika ngazi za Wilaya na ngazi za chini kabisa. Watakwimu hawa ndio watakaotumika kukusanya na kuchambua takwimu katika ngazi hizo. Hata hivyo, kwa sasa watakwimu wa Halmashauri wanashirikiana na wale wa NBS katika kutayarisha takwimu za Pato la Mkoa. TASTA inaendelea kukusanya taarifa za watakwimu wote nchini ili wafahamike wapo wapi na wanafanya nini ili tuweze kuwasaidia katika kuinua viwango vyao katika Tasnia ya Takwimu na mwisho kuwa na lengo moja la kukusanya takwimu bora na kwa wakati. Programu za kuendeleza watumishi (Human development programs) kupitia TSMP itasaidia kuboresha watakwimu hawa wote.

14. ***Swali: How to improve statistical advocacy to address low statistical awareness and inadequate funding? (Challenges and opportunities).***

**Jibu:** Ili kuongeza uelewa kwa wadau kuhusu Takwimu na umuhimu wake, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inajitahidi kujitangaza, kuelimisha na kuhamasisha wadau wake kuhusu takwimu na umuhimu wake katika kupanga mipango ya maendeleo na kufanya maamuzi sahihi. Pia kupitia mpango wa kusambaza takwimu (Dessemination startergy) takwimu zilizokusanywa na kuchambuliwa husambazwa kwa wadau wote katika ngazi zote za utawala mpaka Wilayani.

Tatizo la ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za kitakwimu ikiwa ni pamoja na uhamasishaji, uelimishaji na usambazaji wa takwimu taarifa kwa wadau haliepukiki. Hata hivyo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inajitahidi kutumia fedha kidogo inayopata kutoka Serikalini na kwa wadau wa maendeleo katika kuendesha shughuli zake.

Fursa zilizopo ni pamoja na kuwepo kwa Ofisi za Takwimu katika kila mkoa ambazo zinarahisisha uendeshaji wa shughuli zake katika ngazi za chini. Ofisi hizi zinaongozwa na Mameneja ambao ni watakwimu.

15. ***Swali: Je, takwimu inawasaidia vipi watu wanaoishi vijijini na watoto wanaombaomba mitaani (street children) – Asha Mussa Mahfooudh – EASTC***

**Jibu:** Kazi kubwa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni kutoa picha halisia kwa ajili wa Watunga Sera na taasisi nyinginezo ili ziweze kuchukua hatua stahiki. Takwimu za idadi ya watoto wa mitaani zinaweza

kupatikana kwa kupitia tafiti za kaya binafsi ikiwa ni pamoja na Sensa. Kwa kawaida watafiti wakishakusanya takwimu na kuziwasilisha kwa wadau, ni juu ya hao wadau kuzitumia kwa ajili ya kutunga Sera. Kwa maneno mengine, mtakwimu anatoa viashiria ambavyo humsaidia Mtunga Sera au mpanga mipango kupendekeza nini kifanyike. Hivyo si kazi ya Ofisi ya Takwimu kuwasaidia watoto wa mitaani bali Ofisi inasaidia kutoa takwimu za idadi ya watoto hao na maha ili serli walipo ili Sera stahiki zitungwe na maamuzi sahihi yafanyike kuwasaidia kuwasaidia watoto hao.

***16. Swali: Je, serikali ina mpango gani wa kuanzisha Idara ya Takwimu inayojitegemea katika Wizara? – Wilberforce William (Ujenzi).***

**Jibu**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilizinduliwa rasmi tarehe 26 Machi, 1999 kuwa Wakala wa Serikali (Executive agency) kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997. Hata hivyo, katika kutekeleza kazi zake, Ofisi hii iko chini ya Wizara ya Fedha. Kutokana na Sheria ya Takwimu Na. 1 *(Statistics Act)* ya mwaka 2002, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa jukumu la kuendesha, kusimamia na kuratibu shughuli zote za kitakwimu Tanzania Bara.

***17. Swali: Takwimu ni muhimu, Je, tunaona umuhimu wa kuwa na fungu la hela kwenye mipango ili kuboresha takwimu? Yaani kuwe na fungu ambalo ni muhimu kama sekta nyingine.***

**Jibu:** Kuna fungu kwa ajili ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu bajeti ya Serikali. Hata hivyo, wakati mwingine fedha hiyo haitoshi na hivyo kuna wadau wa maendeleo ambao pia huchangia katika kuhakikisha takwimu zinakusanywa na kuchambuliwa.

***18. Swali: Mtahakikishaje kuwa takwimu zinazokusanywa kila mwaka au baada ya miaka fulani au muda fulani ni za ukweli na hazina uongo au uchakachuaji ndani yake? – Yacintha Yona – Zanaki Sekondari.***

**Jibu:** Ukusanyaji wa Takwimu una taratibu zake, wakusanyaji wa takwimu hupewa semina ya jinsi ya kuzikusanya takwimu hizo ikiwemo jinsi ya kuuliza maswali ili kupata jibu linalotarajiwa. Aidha kila mkusanya takwimu huwa na kiongozi wake ambaye atahakikisha kuwa takwimu zinazokusanywa ni sahihi. Mchakato wa kupitia takwimu hizo huendelea mpaka katika ngazi ya juu kabisa kabla ya kutolewa rasmi kwa ajili ya matumizi.

19. ***Swali: Je, public relation officers wa taasisi wanahusishwaje katika uzalishaji na usambazaji wa takwimu?***

**Jibu**: Afisa Habari wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu anahusishwa katika hatua zote za ukusanyaji uchambuzi na usambazaji wa kitakwimu. Aidha, Afisa Habari ni kiungo muhimu kati ya taasisi na vyombo vyote vinavyotumika kuhamasisha, kuelimisha na kutoa habari kwa wananchi.

***20. Swali: Kuna umuhimu gani wa kuwa na watakwimu kwenye Idara ya Elimu ambapo kazi hiyo inaweza kufanywa na Maafisa Elimu, Kata, Wilaya, Mkoa, nk?***

**Jibu**: Ukusanyaji, uchambuzi, na usambazaji wa Takwimu unatakiwa uzingatie mbinu za kitakwimu kwa kufuata taratibu zilizowekwa ili kupata takwimu bora kwa matumizi ya wakati husika. Watakwimu wanafahamu mbinu hizi za ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu ndio maana wanatakiwa kuwepo katika idara zote ili taarifa za kitakwimu zinazokusanywa ziwe na ubora na ziweze kulinganishwa kimataifa.

***21. Swali: Je, ni juhudi zipi zimefanywa ili kuwezesha somo la Takwimu lifundishwe katika ngazi ya shule ya msingi au sekondari. Hii itasaidia kuongeza uelewa wa jamii katika utumiaji wa takwimu. – Nelson J.R , Ofisi ya Mkuu wa Mkoa***

**Jibu**: Msingi mkuu wa kuwa mtakwimu ni somo la hisabati. Serikali imeendelea kuweka somo la hisabati kama somo la msingi katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari na imeendelea kuwasisitizia wanafunzi umuhimu wa kujua hisabati. Aidha, takwimu za msingi ndani ya somo la hisabati hufundishwa katika ngazi ya sekondari japo si moja kwa moja. Mfano; idadi ya vitu, wingi, wastani, uwiano, n.k. Hivyo kwa msingi uliopo kwa wale wanaopenda kuwa watakwimu bado wana nafasi ya kujiwekea msingi mzuri wa kuwa watakwimu kwa kufanya vizuri kwenye somo la hisabati.

***22. Swali: Kutokana na maelezo yaliyotolewa ina maana kuwa kuna umuhimu wa kukusanya takwimu toka vijijini au mijini kuhusu wanafunzi katika shule, watoto wagonjwa na akinamama / wazee kutoka sehemu mbalimbali? – Rachel Leonce – Zanaki Sec.***

**Jibu:** Ukusanyaji wa takwimu zozote katika nchi zinahusisha maisha ya jamii ya Mtanzania. Sensa ya Watu na Makazi imekuwa ikifanyika kila baada ya miaka kumi ili kupata taarifa za watu na makazi yao. Kuna tafiti za afya ukiwemo Utafiti wa Afya na Uzazi (DHS) ambao pia unaangalia upande wa afya, kuna tafiti za hali ya umaskini (Panel Survey), Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (HBS), tafiti za viwanda na biashara na nyingine nyingi ambazo zinakusanywa taarifa toka vijijini ili kupata takwimu za

kuisaidia serikali katika kupanga mikakati ya kuisaidia jamii ya Tanzania. Hivyo Takwimu za kina mama na watoto, wanafunzi, n.k zinapatikana toka katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

***23. Swali: Nani anaratibu ubora wa Takwimu Tanzania?***

**Jibu:** Kutokana na Sheria ya Takwimu Namba 1 *(statistics act)* ya mwaka 2002, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa mamlaka ya kuendesha, kusimamia na kuratibu shughuli zote za kitakwimu Tanzania Bara. Ofisi hii ndio pekee inayotoa Takwimu rasmi nchini.

***24. Swali: Utajuaje takwimu bora, wakati wahusika wa hizo takwimu wanachelewa kupata mrejesho nyuma wa takwimu zilizokusanywa?***

**Jibu:** Ofisi ya Taifa ya takwimu inajitahidi sana kutoa mrejesho nyuma kwa wadau kutokana na takwimu zilizokusanywa. Inapotokea kuna ucheleweshaji inawezekana kabisa ni katika harakati za kuhakiki ubora wa takwimu zilizowasilishwa kwani wakati mwingine inalazimu kufanya utafiti mdogo ili kuhakiki baadhi ya taarifa zilizokusanywa.

***25. Swali: Kwa kuzingatia vigezo vya takwimu bora – je Tanzania ina hadhi gani katika ukusanyaji takwimu – na matumizi kikanda Afrika? – Ludovick J. Nduhiye – Secretarieti ya Baraza la Mawaziri.***

**Jibu:** Kwa ujumla Takwimu rasmi zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu zina ubora wa hali ya juu kwa sababu zinatayarishwa katika viwango na mbinu za kitakwimu zinazokubalika kimataifa. Pia mbinu zinazotumika kutayarisha takwimu hizo zipo wazi kwa kila mdau kuweza kuzipitia na kuzitumia pale inapobidi ili kuhakiki ubora wa takwimu zinazotolewa. Kwa sasa Tanzania inashiriki katika program mbalimbali za kimataifa kama vile General data dissemination System (GDDS) ambapo mfumo wetu wa utayarishaji, uchambuzi na usambazaji unalinganishwa na nchi nyingine duniani.

***26. Swali: Takwimu za Wizara ya Fedha zinawasaidiaje wajasiriamali wadogo wadogo wanaojiendeleza kiuchumi na zinawafikia vipi wajasiriamali hao?***

**Jibu:** Takwimu zilizopo zinamsaidia kila mdau anayezihitaji kwa matumizi mbalimbali. Mfano katika kitabu cha Hali ya Uchumi kuna takwimu nyingi sana ambazo zinaweza kupatikana kwa miaka kadhaa. Takwimu hizi zikishakamilika huwa zinawekwa katika maktaba zilizopo katika ofisi zote za takwimu ikiwa ni pamoja na zile za mikoani. Watunga Sera na Wapanga Mipango huwa wanazitumia Takwimu hizi kwa kiasi kikubwa. Hivyo hata sera sahihi za ujasiriamali zinaweza kutungwa kwa kutumia

takwimu hizi. Inapotokea kuna takwimu maalum zinahitajika, ofisi huwa inaangalia uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya utafiti kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wadau wake.

***27. Swali: Je? Takwimu zinawasaidiaje watu wenye ulemavu katika kupanga mipango ya nchi? Ramla O.Saidi***

**Jibu:** Takwimu husaidia kutunga Sera na kupanga mipango sahihi ya maendeleo. Utafiti wa Watu Wenye Ulemavu unatoa viashiria muhimu kama vile idadi ya walemavu kwa aina ya ulemavu, umri, mahali wanapoishi, jinsi, n.k. Kwa mfano; endapo utafiti utabaini kuwa watu wengi wenye ulemavu wa viungo wapo eneo fulani basi serikali inabidi ijipange jinsi ya kuwasaidia kwa kuangalia vipaumbele. Bila takwimu serikali au mashirika ya misaada hayataweza kujua ianzie wapi kutoa misaada kwa walengwa.

***28. Swali: Takwimu ambazo sio "National Aggregate" zitaanza kutoka lini?***

**Jibu:** Takwimu nyingi zinazotokana na Sensa na tafiti mbalimbali zinatolewa kimkoa na kiwilaya mfano Sensa ya Watu na Makazi, Tafiti za Kilimo na Mifugo, n.k. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inajua kuwa inakabiliwa na changamoto ya kutoa takwimu ambazo sio za kitaifa, kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Hata hivyo kila inapopatikana fedha ya kutosha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu hutoa takwimu hizo ambazo kwa sasa mahitaji yake ni makubwa.

***29. Swali: Je, takwimu inasaidia vipi wakati wa sensa kuhesabu idadi ya watoto wanaoishi mitaani ambao hawana sehemu maalum ya makazi na je inasaidiaje katika kupunguza idadi ya watoto hawa. – Reslina R .Paul – Zanaki Sekondari***

**Jibu:** Wakati wa Sensa ya Watu na Makazi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu huweka utaratibu maalum wa kuhesabu watu wote wasio kuwa na makazi na makazi maalum wakiwemo watoto wa wanaoishi mitaani. Takwimu hizi zinatumiwa na Serikali kupitia Wizara inayoshughulika na maswala ya watoto wasio na makazi maalum katika kupanga mipango ya kuondoa changamoto hizo za watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

***32 Swali: Integrated labour force survey inatarajiwa kufanyika lini; takwimu zilizopo zimepitwa na wakati.***

**Jibu:** Utafiti huu uko kwenye hatua za mwisho za maandalizi na utafanyika mwaka 2014.

***30. Swali: Kiukweli wanafunzi wanaosomea taaluma ya takwimu ni wachache sana na hata vyuo ni vichache. Je, mnatuhakikishiaje kuwa kufikia 2025 kutakuwa na watakwimu wa kutosha kukusanya takwimu kila kona nchini? – Mwalimu- Zanaki sekondari.***

**Jibu:** Inavyoonekana kwa sasa wanafunzi wanaosomea taaluma ya takwimu ni wachache, lakini baada ya miaka 10 inawezekana kabisa kukawa na watakwimu wengi kwa sababu Serikali kupitia Chuo cha Takwimu mashariki mwa Afrika (EASTC) na vyuo vingine vinavyotoa taaluma ya takwimu vinajipanga kuongeza idadi ya wanataaluma ya Takwimu. Mfano Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kina mpango wa kupanua huduma zake ili kiweze kutoa wahitimu wengi wa shahada ya kwanza na ya pili. Pia, kupitia Mpango kabambe wa kuboresha Takwimu (TSMP), watakwimu waliopo katika Halmashauri watajengewa uwezo ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kitakwimu katika ngazi za chini. Ofisi ya Taifa ya takwimu inasisitiza na kuhamasisha wanafunzi wakazanie somo la hisabati ili wajiwekee mazingira mazuri ya kuwa watakwimu wa baadaye. Ni dhahiri kwamba kama kutakuwa na uhamasishaji wa kutosha kuanzia kwa wanafunzi wa madarasa ya chini, na kama wanafunzi wanaomaliza sekondari wataelimishwa na kuhamasishwa vya kutosha kuhusu tasnia ya takwimu na manufaa yake kwa Taifa, inawezekana kabisa hadi kufikia 2015 wakawepo watakwimu wa kutosha. Tunawaomba Walimu wawe wahamasishaji wakuu katika hili hasa tukizingatia kuwa kila mtu ni mdau wa Takwimu.

***31. Swali: Je serikali ina mikakati gani ya upatikanaji wa watakwimu bora ikiwa chuo kinachotoa mafunzo ya takwimu ni kimoja? – Mwanafunzi EASTC.***

**Jibu:** Watakwimu bora husaidia kutoa takwimu bora na hao watakwimu bora hutoka katika vyuo vinavyotoa mafunzo bora ya takwimu. Ieleweke kwamba, Chuo cha takwimu ni kimoja lakini kuna vyuo vingine kama Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Mzumbe na Chuo Kikuu cha Dodoma ambavyo navyo huzalisha watakwimu wazuri. Inawezekana kabisa nchi ikawa na chuo kimoja na kikaweza kuzalisha watakwimu wengi na bora, kwani hili ni suala la kimkakati. Isitoshe, Somo la takwimu limejumuishwa kwenye mitaala ya vyuo vingi vya elimu ya juu na hivyo mtakwimu bora si lazima atoke katika chuo cha takwimu bali anaweza kutoka katika chuo kingine na akaongezewa mafunzo kwa vitendo na akaweza kuzalisha takwimu bora. Kwa sasa, Serikali inajitahidi kuimarisha, kupanua na kuviwezesha vyuo vinavyotoa taaluma ya takwimu ili viweze kuzalisha watakwimu wengi.

***32. Swali: Chama cha Watakwimu wanatoa elimu gani ya uhamasishaji kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ili waweze kusoma takwimu? Mary August – Ofisi ya waziri mkuu.***

**Jibu:** Chama cha Watakwimu (TASTA) kilianzishwa kwa lengo la kuwaunganisha watakwimu wote nchini ili waweze kushirikiana katika kuitangaza Tasnia ya Takwimu. TASTA inatumia mikutano mbalimbali kuwahamasisha wanafuzi waweze kusoma takwimu. Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika ni mojawapo ya mikusanyiko ya watakwimu ambapo TASTA hupewa nafasi ya kuwasilisha mada ili kuitangaza na kuwahamasisha wanafunzi wa sekondari na vyuo ambao hualikwa kwenye maadhimisho haya.

**33. Swali: Mnafikiri watunga Sera wanazifanyia kazi tafiti za watafiti kama wale wa REPOA na ESRF**?

**Jibu:** Takwimu zipo nyingi na za aina mbalimbali. Vyanzo vya takwimu ni pamoja na tafiti ambazo hufanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu au Taasisi nyingine za utafiti kama REPOA NA ESRF.
Watunga sera nchini wana uhuru wa kutumia chanzo chochote cha takwimu pamoja na ukweli kwamba Ofisi ya Taifa ya Takwimu ndio taasisi pekee inayotoa takwimu rasmi nchini. Takwimu za Taasisi nyingine mara nyingine hutumika pale ambapo takwimu inayohitajika haipatikani katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

***34. Swali: Ofisi ya Takwimu imejipanga vipi kuhakikisha kwamba takwimu zinafika kwenye idara husika na zinafanyiwa kazi?***

**Jibu:** Mara tu matokeo ya awali yanapopatikana Ofisi ya Taifa ya Takwimu huwa inatoa machapisho na pia inatangaza matokeo hayo kwa wadau wote kupitia vyombo vya habari, kuweka matokeo hayo katika tovuti ya taasisi, kuweka matokeo hayo katika maktaba ya Ofisi pamoja na kusambaza machapisho yenye matokeo hayo kwa idara zote za serikali. Kwa maana hiyo takwimu huwa zinafika katika idara husika. Kuhusu kufanyiwa kazi na Idara husika, ofisi ya Taifa ya Takwimu huwa inafanya utafiti wa wadau kuona kama wanaridhika na Takwimu zinazotolewa na Ofisi, hivyo Ofisi ya Taifa ya takwimu inaweza kujua kama takwimu hizo zinafanyiwa kazi au hapana kupitia matokeo ya utafiti huo.

***35. Swali: Sekta ya Habari na Teknohama (ICT) haijawahi kufanyiwa utafiti rasmi wa kitaifa katika "household level". Je Ofisi ya Taifa ya Takwimu wana mpango gani wakizingatia sekta hii inakuwa kwa kasi sana. – TCRA.***

**Jibu:** Ni kweli kuwa sekta ya habari inakua kwa kasi kubwa ikilinganishwa na sekta nyingine za uchumi lakini hakuna utafiti wa peke yake uliowahi kufanywa na Ofisi ya taifa ya Takwimu ila katika tafiti mbalimbali za kaya kama ule wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) huwa kuna swali linalogusia ICT. Kwa kuwa huu sio utafiti wa ICT peke yake, inawezekana kabisa taarifa za ICT zinazotokana na utafiti huu hazikidhi matakwa ya wadau wa sekta hii. Hivyo hii ichukuliwe kama ni changamoto kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kushirikiana na TCRA na wadau wengine wa habari nchini ili kuangalia namna ya kupata taarifa zinazohitajika. Ikumbukwe kwamba Ofisi ya Taifa ya takwimu inafanya tafiti kulingana na matakwa ya wadau na si vinginevyo.

***36. Swali: Kwa nini Serikali ya Tanzania imeshindwa kukuza sekta ya uvuvi hasa ule wa uzalishaji wakati vyanzo vya maji vipo? na takwimu za vyanzo vya maji zipo?***

**Jibu**: Sekta ya Uvuvi ni mojawapo ya sekta muhimu ndani ya sekta kuu ya kilimo. Tanzania tumebahatika kuwa na vyanzo vingi vya maji lakini yamekuwepo malalamiko mengi toka kwa wadau kuwa Serikali haitumii vizuri rasilimali tulizonazo ili kukuza sekta ndogo ya Uvuvi. Mojawapo ya changamoto zinazoikabli sekta ya Uvuvi ni ukosefu wa takwimu za kutosha. Chanzo kikuu cha takwimu ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati imekuwa ni changamoto hata kwa Wizara yenyewe hasa tukizingatia uzalishaji katika sekta hii unavyofanyika. Ni rahisi kidogo kupata takwimu kwa wavuvi wakubwa lakini kwa wale wavuvi wadogo na wa kati imekuwa changamoto kupata takwimu za kutosheleza. Hata hivyo baadhi ya takwimu zinapatikana katika kitabu cha hali ya uchumi kinachotayarishwa kila mwaka na Wizara ya Fedha.

***37. Swali: Serikali na hasa wanasiasa wamekuwa wakiweka tafiti makabatini bila kuzitumia katika kufanya maamuzi. Je, ni kwa kiasi gani REPOA mmepigania hali hii ipungue ili wataalamu watumike kuleta maendeleo?***

**Jibu:** REPOA kama taasisi ya Utafiti kwa nafasi yake imekuwa ikifanya tafiti mabalimbali na imekuwa ikihamasisha matumizi ya takwimu katika kupanga mipango ya maendeleo. Katika maelezo yangu ya awali nimetoa mfano mmoja kwamba nilitembelea Wilaya moja na nikaambiwa na viongozi wa Wilaya hiyo kuwa wanategemea uchumi wa Wilaya yao utakua kwa asilimia 10, lakini nilipouliza endapo wana

takwimu zozote zinazoonesha hali halisi ya sasa walijibu hawana takwimu. Nikajiuliza malengo ya ukuaji wa asilimia kumi yametokana na nini sikupata jibu. Hivyo nazidi kuhamasisha elimu ya juu ya utoji na utumiaji wa takwimu itolewe katika ngazi zote za kiutawala kwa ajili ya kupanga mipango na kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

***38. Swali: Katika ukusanyaji wa takwimu baadhi ya watu hupuuzia utoaji wa takwimu hizi. Je sisi kama watakwimu tunachukua hatua gani ili tupatiwe takwimu kwa urahisi, na sheria inasema utoaji wa takwimu ni hiari. Tukiendelea kutumia sheria hii, haiwezi kufikia hatua ya watu kukataa kutoa takwimu kabisa?***

**Jibu:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mamlaka ya kisheria iliyo nayo ina uwezo wa kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote anayekataa kutoa takwimu. Lakini mara nyingi kabla ya kuchukua hatua ya kumshitaki mtoa taarifa, huwa inajitahidi kutumia busara zaidi kwani inaamini kuwa wakati mwingine mdau anaweza kukataa kutoa taarifa kwa kutokujua maana na sababu ya yeye kuhitajika kutoa takwimu hizo. Njia ya kidiplomasia inaposhindikana, ndipo hatua zaidi huchukuliwa kwa kumpeleka mtu huyo kwenye vyombo vya sheria. Ofisi ya Taifa ya Takwimu ipo kwenye mchakato wa kuboresha Sheria ya Takwimu ya mwaka 2002 ili kupunguza au kuondoa kabisa uwezekano wa kukosa taarifa pale zinapohitajika.

***39. Swali: Takwimu zinatafsiriwa vipi kiuhalisia? Mfano – utasikia uchumi umekuwa kwa asilimia fulani lakini hali hiyo haionekani kwani wananchi wanalia hali ni mbaya – umaskini***

**Jibu:** Kwa lugha rahisi kukua kwa uchumi inamaanisha kupanuka kwa shughuli za uzalishaji wa huduma na bidhaa nchini katika kipindi fulani. Kupanuka kwa uzalishaji kunaweza kuchangiwa na kuongezeka kwa idadi ya wazalishaji au kuboreshwa kwa huduma inayotolewa. Hii ina maana hakuna njia ya kukuza uchumi bila kushiriki kwenye uzalishaji. Kama ni mkulima basi anatakiwa ashiriki kikamilifu kwenye kilimo ili mwisho wa mwaka avune zaidi ya alichovuna mwaka jana. Soko likiwa zuri basi mkulima huyu akiuza mazao yake atapata kipato kitakachomsaidia kupunguza makali ya maisha na Mkulima huyo huyo atalia hali mbaya endapo hajashiriki kwenye kilimo au ameshiriki lakini hajavuna chochote au amevuna kidogo ikilinganishwa na alichovuna mwaka jana.

Ikumbukwe kuwa katika kutayarisha takwimu za pato la Taifa, tunaangalia ukuaji wa uchumi jumla (macroeconomy) ambao unawajumuisha wazalishaji wote kwa ujumla wao. Mkulima anaweza kushuka kiuzalishaji lakini kipindi hicho hicho uzalishaji katika sekta nyingine ukakua na hivyo kusababisha

uchumi kwa ujumla ukakua kwa mwaka huo ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Kwa nchi kama Tanzania, unaweza kukuta takwimu zinaonesha uchumi umekua lakini mwananchi wa kawaida ni masikini sababu sekta zinazokua sana ni zile ambazo hazimgusi mwananchi wa kawaida moja kwa moja, mfano mawasiliano, na sio kilimo ambacho kimeajiri mwananchi walio wengi.

***40. Swali: Kila Mtanzania ana haki ya kupata ajira, tunapoongelea upatikanaji wa ajira katika sekta ya ajira nchini. Je, kitaaluma, kwa kutumia takwimu, Tanzania imepiga hatua gani kuhakikisha kwamba kuna ongezeko la ajira nchini? –John Paul – EASTC***

**Jibu:** Kimsingi, watu wenye uwezo wa kufanya kazi ni raslimali muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Nguvukazi hii isipotumika kikamilifu, ni hasara kubwa kwa ustawi wa jamii yetu, Kwa kuliona hilo, serikali na wadau wengine wa maendeleo nchini wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha upatikanaji wa ajira unaongezeka kulingana na mahitaji ya ajira yalivyoongezeka.